

Mwafrika 22/4/63

Kuzaliwa kwa umoja Msumbiji

MWANDISHI

Rais wa Frelimo, Dr. Eduardo C. Mondlane ndiye Mwandishi wa kumbukumbu hii ndefu kuhusu Msumbiji ambayo inatolewa katika gazeti hili kwa vipande vipande hadi mwisho. Usikose kipande cho chote ili ufahamu jinsi Mreno anavyofanya Msumbiji.

TUKIENDELEA na masilimuzi ya Ukoloni ya Kireno katika Msumbiji, leo Rais wa Frelimo, Dr. E. Mondlane, anaeleza jinsi wananchi wa Msumbiji walivyotoka nje ya nchi yao na kuanzisha vyama vya siasa katika nchi za majirani ili kupigania uhuru wa nchi yao. Dr. Mondlane anasema:

"Mpaka hivi sasa nimesimulia tu jinsi siasa za utafa zilivyojaliwa katika nchi ya Msumbiji. Lakini hivi sasa ninataka kueleza kwa kifupi jinsi vyama vipya vilivyoundwa kwa madhumuni hasa ya kupigania uhuru wa Msumbiji.

"Mozambique Liberation Front, au kwa kifupi Frelimo) Frente de Liberacao

de Mozambique, ni chama kipya cha siasa kilichoundwa mwezi Juni mwaka jana. Chama hicho kiliundwa kwa kuunganisha vyama mbalimbali, vingine vikiwa vya watoro wa Msumbiji na vingine nje vile vinavyoendesha kwa siri katika Msumbiji yenyewe.

"Kwa sababu ya usalama, sitaeleza hapa habari za vyama hivyo vinavyoendesha kwa siri katika Msumbiji, isipokuwa nitasema kuwa vyama hivyo vinatumika kama silaha ya kuhimiza umoja miongoni mwa vyama vyote vinavyopigania uhuru.

"Nikipotembelea Msumbiji mwaka 1961 nikiwa Mjumbe wa UNO, niliombwa kujizulu katika idara ya UNO inayosimamia nchi za udhamini ili nifike Afrika ya Mashariki kujaribu kuunganisha vyama vyote vya watoro katika juhudi ya kupigania uhuru kwa sauti moja.

"Vyama marufu vya wakimbizi vilivyoko sasa katika Frelimo ni Mozambique African National Union (Manu) na Union National Democratica de Mozambique (Udenamo).

(Inaendelea uk 6)

CHANZO CHA UMOJA → WA² MSUMBIJI

(Inatoka uk 5)

Waanzishaji wa Manu niwananchi wa Msumbiji waliokuja kufanya kazi katika Afrika ya Mashariki Tanganyika, Kenya na Uganda. Miongoni mwa wanachama wa Manu, walihusika pia na siasa za nchi hizi za Afrika ya mashariki.

"Ilipojulikana kuwa Serikali za Afrika ya Mashariki zilikapidhiwa mikono ni mwa Waafrika, wananchi hao wa Msumbiji, waliona ni lazima nao wajitahidi kupigania uhuru wa kwao. hivyo ndivyo alivyokuwa Bw. Matthew Mmole, aliyekuwa Rais wa Manu. Katibu Mkuu wa zamani wa Manu, Bwana M.M. Mallinga aliyekuwa Afrika ya Mashariki kwa miaka mingi akiongoza vyama vya wafanya kazi katika Kenya, Uganda na Tanganyika, alitia moto mwingine katika siasa, hasa juu ya mambo ya wafanya kazi. (Bw. Mallinga au Millinga, ni mwananchi wa Tanganyika).

"Kwa upade mwingine Wasumbiji wengine walio-kuwa wakifanya kazi

katika nchi za Rhodesia na Nyasaland pia walijiunga katika vyama.

"Huko Rhodesia na Nyasaland ndiko kulikoanza Udenamo. Kwanza Udenamo ilikuwa na makao makuu yake Salisbury, Rhodesia ya Kusini.

Vile wananchi wa Rhodesia waliruhusiwa kuendesha vyama vyao, pia, Wasumbiji waliendelea na juhudi yao bila taabu. Nilipopita Salisbury mapema mwaka 1961, nilikuta makundi mengi ambayo wakati mwingine wakishirikiana na wakati mwingine yakitengana.

"Nilijitahidi kuwashauri wajiunge pamoja ili wapate kushirikiana na vyama vingine vya Msumbiji na vya watoro.

"Kiongozi mmoja wa Udenamo alikuwa Adeline Grambe, mwenye umri wa miaka 23, ambaye kadiri ya historia yake, alikuwa katika jeshi la siri la Polisi ya Kireno inayoogopewa sana (PIDE).

"Inasadikiwa kuwa Bw. Grambe alitumwa na Serikali ya Kireno kupeleleza mambo yanayofanywa na wananchi wenzake wa Msumbiji katika nchi ya Rhodesia.